



RIPOTI YA KIHAIIDROLOJIA JARIDA LA MWEZI

BWAWA JULIUS NYERERE (JNHPP)

MEI, 2026

Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00



"KILA TONE LINATHAMANI"


Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00

Muhtasari wa Hali ya Maji

Bwawa la Julius Nyerere Hydropower Plant (JNHPP) hupokea maji kutoka mito mikuu mitatu: Great Ruaha, Kilombero na Luwegu, ambayo ni sehemu ya Bonde la Rufiji. Mito hii ni muhimu kwa uzalishaji wa umeme wa maji, kilimo, matumizi ya majumbani na ikolojia.

Katika mwezi Mei 2026, viwango vya maji vilikuwa juu ya wastani kwa asilimia 183 ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa mwezi husika. Hali hii ilisababishwa na wastani wa mvua iliyonyesha katika ukanda wa juu wa vidakio vitatu pamoja na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji.

Aidha, usawa wa maji katika bwawa la JNHPP mpaka kufikia Mei 31 ulikuwa juu wastani kwa asilimia 100.09 ukilinganisha na wastani wa muda mrefu kwa mwezi husika. Zoezi la kupunguza maji bwawa la Julius Nyerere bado linaendelea na limechukua takribani siku 46. Jumla ya mita za ujazo billioni 6.5 sawa na asilimia 33.51 ya ujazo wa bwawa Hifadhi Hai (Bilioni 19.4 mita za ujazo) zimepunguzwa kufikia tarehe 31 Mei 2026.



Hali ya Hewa

Hali ya Mvua – Mei 2026:


Takwimu za mvua zilizorekodiwa na vituo vya hali ya hewa katika maeneo mengi ya Bonde la Rufiji zilikuwa za wastani hadi chini ya wastani, hali hii inachangia kuanza kupungua kwa mtiririko wa maji katika baadhi ya mito hususani ile inayotiririsha maji kwa msimu wa mvua tu.

Mwelekeo wa Hali ya Hewa – Juni 2026:


Kwa mujibu wa utabiri wa hali ya hewa uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA):

- Unatarajiwa kuwa na vipindi virefu vya ukavu katika maeneo mengi ya Bonde la Rufiji, huku mvua nyepesi zikiendelea kujitokeza mara kwa mara katika maeneo ya Mashariki (Dar es Salaam, Pwani, na sehemu za Morogoro).
- Hali ya joto la wastani hadi baridi kali itaambatana na ukavu katika maeneo ya Kusini na Kati ya bonde.


Utabiri wa Mvua
Wiki 01 Juni, 2026




Utabiri wa Mvua
Wiki 02 Juni, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 03 Juni, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 04 Juni, 2026



Hali ya Mtiririko wa Maji

Vituo vya Kihaidrolojia


Wingi wa maji mitoni katika kipindi cha mwezi Mei 2026 uliendelea kuwa juu ya wastani wa muda mrefu. Takwimu za vituo vya ufuatiliaji zinaonesha ongezeko la mtiririko ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu kwa mwezi husika (LTA: 2000–2025).

Matokeo ya Kihidrolojia


Hali ya wingi wa maji yanayoingia katika Bwawa la Julius Nyerere imeonyesha kupungua katika kipindi cha Mei kuelekea Juni. Hata hivyo, kiwango hicho kimeendelea kuwa himilivu kwa kuwa usawa wa maji katika bwawa uko juu ya wastani wa muda mrefu. Hali hii inaashiria mtiririko thabiti wa mito unaosaidia kupunguza hatari ya kupungua kwa kina cha bwawa na kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa umeme

Jedwali 1: Mchanganuo wa Takwimu za Wingi wa Maji (Mei, 2026)

Na	Namba ya Kituo	Mto	Wastani Wingi Mei 2026 (m³/s)	Wastani Wingi wa Maji LTA Mei 2000–2025 (m³/s)	Maelezo
1	1KA3B	Great Ruaha at Msolwa	205.39	101.75	Juu zaidi ya Wastani
2	1KB17	Kilombero at Swero	1402.02	684.33	Juu zaidi ya Wastani
3	1K3C	Luwegu at Mbarang’andu	42.68	30	Juu ya Wastani



Hali ya Maji Bwawani



Katika mwezi Mei 2026:

Hali ya usawa wa maji katika Bwawa la Julius Nyerere bado uliendelea kuimarika licha ya mvua kusimama. Hali hii imechagizwa na utunzaji wa vyanzo vya maji, usimamizi wa rasilimali za maji pamoja na wingi wa mvua (wastani mpaka juu ya wastani) zilizorekodiwa kipindi cha masika 2026 katika vidakio vya Great Ruaha, Kilombero na Luwegu.

Uchambuzi

Zoezi la kupunguza maji bwawa la Julius Nyerere bado linaendelea na limechukua takribani siku 46. Jumla ya mita za ujazo bilioni 6.5 sawa na asilimia 33.51 ya ujazo wa bwawa Hifadhi Hai (Bilioni 19.4 mita za ujazo) zimepunguzwa kufikia tarehe 31 Mei 2026.

Mapendekezo

- Kuendelea na Usimamizi shirikishi wa Rasilimali za Maji kuelekea kipindi cha Kipupwe hii itasaidia katika usimamizi thabiti na endelevu wa Bwawa la Julius Nyerere pamoja na shughuli za kijamii.
- Kuhakikisha kiwango cha maji kinabaki ndani ya viwango vya juu vya uzalishaji umeme ili kuendeleza uzalishaji wa umeme wa maji kwa ufanisi na matumizi mengine ya maji.

